**JAMHURI YA MUUNGO WA TANZANIA**

**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

**MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A**

**650** **HAIBA NA MICHEZO**

**Muda: Saa 3 Hours** **Mwaka: 2024**

---

**Maelekezo**

1. Karatasi hii ina Sehemu **A** na **B** zenye jumla ya maswali **kumi na manne (14).**
2. Jibu maswali **yote** kutoka Sehemu **A** na maswali **manne (4)** kutoka Sehemu **B**.
3. Sehemu **A** ina alama **arobaini (40)** na Sehemu **B** ina alama sitini **(60).**
4. Simu za mkononi **haziruhusiwi** ndani ya chumba cha mtihani.
5. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

maktaba.tetea.org
TETEA


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

**SEHEMU A (Alama 40)**

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

1. Eleza stadi tano ambazo mwalimu wa somo la Haiba na Michezo anatakiwa kuwa nazo katika kubuni, kufaragua na kutengeneza zana za kufundishia na kujifunzia.
2. Fafanua changamoto tano anazoweza kukutana nazo mwalimu ambaye hatatumia kitabu cha kiada katika maandalizi ya ufundishaji wa somo lake.
3. Eleza mambo matano yanayopaswa kuzingatiwa wakati wa kuchezesha mchezo wa mpira wa kikapu.
4. Chambua misingi mitano ya kuzingatia katika ufundishaji wa somo la Haiba na Michezo.
5. Eleza kwa ufupi mambo ya msingi manne anayopaswa kukumbuka mwalimu anapotumia muhtasari wa somo la Haiba na Michezo katika ufundishaji.
6. Fafanua kwa kifupi faida nne ambazo shule inazipata kutokana na upimaji wa maendeleo ya mwanafunzi katika somo la Haiba na Michezo.
7. Eleza kwa kifupi manufaa manne atakayopata mwalimu kwa kuandaa Azimio la Kazi.
8. Ainisha tofauti mbili kati ya stadi binafsi na stadi za timu katika michezo.
9. Eleza kwa kifupi madhara manne ya kufundisha bila kuzingatia Andalio la Somo.
10. Bainisha faida nne za kutunza zana za kufundishia na kujifunzia.

**SEHEMU B (Alama 40)**

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

11. Tumia hoja nne kuainisha umuhimu wa Kiongozi cha Mwalimu.
12. Tumia hoja nne kueleza kwa ufupi umuhimu wa kuwapa wanafunzi majaribio na mazoezi katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji.
13. Chambua kwa ufupi mambo manne ya kiusalama yanayopaswa kuzingatiwa kabla ya kuanza kwa mchezo wa soka.
14. Eleza kwa kifupi manufaa manne ya ujazaji wa shajara ya somo katika ufundishaji wa somo la Haiba na Michezo.


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org